



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

WIZARA YA MADINI

Jarida la

MADINI & UCHUMI

Online Bulletin

(ISSN) 3108-8759: MADINI NA UCHUMI ONLINE NEWS BULLETIN

(ISSN) 3108-8767: MADINI NA UCHUMI ONLINE NEWS BULLETINE

www.madini.go.tz

Toleo Na. 1

Okt. 2025


Jarida Mtandaoni



TATHMINI SEKTA YA MADINI


Kukua na mchango wa Sekta ya madini katika pato la Taifa (GDP)

Na	Mwaka	Kukua kwa Sekta ya Madini (%)	Mchango wa Sekta ya Madini (%)
1	2009	1.2	3.3
2	2010	2.7	3.3
3	2011	2.2	3.3
4	2012	7.8	3.7
5	2013	3.9	4.2
6	2014	9.4	3.7
7	2015	9.1	4.0
8	2016	11.5	4.8
9	2017	5.3	4.8
10	2018	5.1	5.1
11	2019	17.7	5.2
12	2020	6.7	6.7
13	2021	9.4	7.3
14	2022	10.9	9.0
15	2023	11.3	9.1
16	2024	8.3	10.1



TATHMINI SEKTA YA MADINI

Miradi 17 ya Madini iliyofikia hatua za juu za Maendeleo



■ Soko la Madini Geita lilianza kufanya kazi Machi 2019 likifuatiwa na Soklo la Madini Chunya Mei 2021

CHANZO: Bodi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

TAHARIRI



TUNACHOKISEMA, TUNATEKELEZA



Anthony P. Mavunde (MP)
Waziri wa Madini

Kwa kipindi kifupi cha kuanzia Julai hadi sasa, Sekta ya Madini imeonesha kasi ya utekelezaji, uwajibikaji na dhamira ya kweli kuifanya kuwa mhimili mkuu wa uchumi wa nchi. Kupitia vipaumbele, mikakati na maelekezo ya viongozi wakuu wa kitaifa wakiongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumeshuhudia hatua kubwa zinazofungua ukurasa mpya wa maendeleo kupitia Sekta ya Madini.

Kuanzia uzinduzi kiwanda cha majaribio cha uchenjuaji wa madini ya Urani Namtumbo- Ruvuma uliofanyika mwezi Julai, 2025 ni ishara ya Tanzania kujiimarisha katika soko la kimataifa la nishati mbadala.

Pia, uzinduzi wa viwanda vya kusafisha na kusindika madini ya copper na nikeli jijini Dodoma na Chunya unaashiria dhamira ya kuongeza thamani ya madini mkakati hapa, hapa nchini.

Aidha, tukio la kusainiwa Mkataba wa nyongeza wa mradi mkubwa wa uchimbaji madini ya dhahabu wa Nyanzaga, Wilayani Sengerema ambalo limeongeza umiliki wa hisa za Serikali kutoka asilimia 16 hadi 20 za sasa, imethibitisha dhamira ya Serikali kuhakikisha rasilimali madini zinawanufaisha wataanzania na taifa kwa kiwango kikubwa.

Kadhalika, matukio ya uwekaji mawe ya msingi kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) mkoani Dodoma na Geita ni kishahio tosha cha dhamira ya kuifanya Tanzania inakuwa kinara wa Sekta ya Madini Afrika. Maabara hizi za kisasa zinaratajiwa kutoa huduma za uchunguzi wa sampuli za kimaabara kwa ubora na haraka kwa wadau wa Sekta ya madini na na hivyo kuwa mkombozi mkubwa kwa wadau kwa kupata taarifa sahihi za kimaabara na hatimaye kuchochea uwekezaji zaidi.

Aidha, kukabidhiwa kwa leseni ya utafiti kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika eneo la Wigu Morogoro ni vielelezo vya uwekezaji wa Wizara katika kwa taasisi zake, ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na usimamizi wa rasilimali.

Mpaka sasa tuna miradi mbalimbali ya kimkakati ukiwemo mradi wa **Faru Graphite** wenye thamani ya takribani shilingi Trilioni 1.3

Haya yote ni ushahidi kwamba tulichokipanga, tunakitekeleza kwa bidii na tija. Katika mwaka huu wa fedha 2025/26, Wizara inaendelea na dhamira yake ya kuhakikisha kuwa vipaumbele vya Wizara vinatekelezwa kikamilifu. Lengo kuu ni kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa taifa kutoka asilimia 10.1 ya mwaka 2024, kukuza ajira kupitia shughuli za madini, kuongeza mapato ya Serikali yanayotokana na madini, na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Kwa kumaliza niseme tu, kama Sekta tumeanza safari ya mageuzi, na hakuna kurudi nyuma.

#Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri



TAHARIRI

TUNAONGEZA BIDII, TUNAVUNA MAFANIKIO



Eng. Yahya I. Samamba
Katibu Mkuu, Wizara ya Madini

Wizara ya Madini inaendelea na utekelezaji wa vipaumbele vyake ilivyojipangia kwa Mwaka wa Fedha 2025/26. Kama wasimamizi na watekelezaji wa Sera na Sheria ya Madini, tunajivunia kuona mikakati inayotekelezwa ikizaa matokeo halisi. Dhamira yetu ni kuhakikisha kuwa kila lengo la maendeleo linalopangwa, linatafsiriwa kwa vitendo, kwa wakati, na kwa matokeo yanayogusa maisha ya wataanzania na Taifa.

Katika mwaka wa Fedha 2025/26, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vyote vilivyopangwa. Hii inajumuisha kuimairisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;

kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini muhimu na mkakati; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani madini; kuimarisha uendeshaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za madini kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya wizara.

Katika kuendeleza mchango wa Sekta ya Madini kwenye maendeleo ya nchi tumeweka msisitizo kwenye kuhuisha Sera na Kanuni mbalimbali ili ziendane na mahitaji ya sasa na yajayo ya kiuchumi na kiteknolojia. Tunalenga kujenga mazingira shindani ya uwekezaji, kuimarisha usimamizi wa rasilimali, na kuhakikisha madini yanawanufaisha wananchi moja kwa moja.

Moja ya hatua za kimkakati ni ununuzi wa helikopta kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), kwa ajili ya kuharakisha tafiti za Kina kupitia vision 20230; Madini ni Maisha na Utajiri. Hii ni nyenzo muhimu ya kuongeza ufanisi katika kugundua maeneo mapya ya madini, kuongeza hifadhi ya taarifa za kijiolojia, na kuvutia wawekezaji zaidi kutoka ndani na nje ya nchi.

Pia, tunaendelea kutekeleza kwa vitendo mpango wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo kupitia mafunzo, teknolojia, mitaji na fursa za masoko.

Hili ni kundi lenye mchango mkubwa kwenye ajira na mapato, hivyo tunalilea kwa mkakati wa kulifanya kuwa sehemu rasmi ya uchumi wa taifa.

Ushirikishwaji wa wadau ni msingi wa mafanikio ya Sekta ya Madini, Wizara inaendelea kufungua milango ya kupokea maoni ya makundi yote -kutoka kwa wachimbaji, wawekezaji, wanataaluma hadi jamii -na kuyachambua kwa lengo la kuyafanyia kazi kisera na kiutendaji. Ushirikiano huu ndio nguzo ya mageuzi tuliyonayo.

Tumejipanga kwa mikakati, tunatekeleza kwa vitendo, na tunalenga matokeo. Sekta ya Madini inazidi kuwa mhimili wa uchumi wa nchi, na kama Wizara, tutaendelea kuhakikisha kuwa dhamira hiyo inafikiwa kwa vitendo ikiwemo kuendelea kuhamasisha uwekezaji zaidi katika nchi na nje ya nchi.

"Tunajiimarisha Kufanikiwa Zaidi"

#Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri



NYANZAGA YAANZISHA ENZI MPYA SEKTA YA MADINI

Na Asteria Muhozya



Hivi karibuni Tanzania ilifungua ukurasa mwingine mpya katika historia ya maendeleo ya Sekta ya Madini kupitia mradi wa dhahabu uchimbaji Mkubwa wa Madini ya dhahabu wa Nyanzaga, uliopo Sengerema, mkoani Mwanza. Mradi huu kupitia Kampuni ya ubia ya Sotta Mining Corporation, unatarajiwa kuanza uzalishaji wake wa kwanza **katika robo ya kwanza ya mwaka 2027.**

Kinachofanya Nyanzaga kuwa wa kipekee ni ukweli kwamba **ni uwekezaji mkubwa katika uchimbaji wa dhahabu nchini ndani ya kipindi cha zaidi ya miaka 10,** ikitoa ishara tosha kwamba Tanzania imejenga mazingira imara na ya kuvutia wawekezaji, na sasa inatambulika kama **kimbilio salama na lenye uhakika kwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini.**

Kupitia mkataba wa nyongeza ulisainiwa Agosti 20, 2025 kati ya Serikali na Kampuni ya Sotta Mining Corporation umeongeza hisa za Serikali katika mradi huo kutoka asilimia 16 ya awali kufikia asilimia 20 ya sasa hatua inayooneshwa msimamo wa Serikali kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa kweli na manufaa kwa wananchi.

Kipaumbele cha Kitaifa Vipaumbele vya Wizara Vyaanza Kuzaa Matunda

Kwa miaka kadhaa mfululizo Wizara ya Madini imekuwa ikirejea kipaumbele chake cha kuhamasisha

uwekezaji na uongezaji thamani madini kwenye hotuba zake za Bajeti na hata kwa mwaka 2025/26 kipaumbele hiki kimerejelewa ikiwa ni ishara ya wazi kuhakikisha kipaumbele hicho kinatekelezwa kwa vitendo.

Mlango wa Migodi Mikakati Unafunguka

Nyanzaga ni mwanzo tu wa mageuzi makubwa. Tanzania inaendelea kuvutia miradi mingine mikakati ya madini, hususan kwenye madini muhimu ya teknolojia kama **graphite, nickel, rare earths, na kobalti.** Miradi hii inaiweka Tanzania kwenye nafasi ya kipekee katika soko la dunia la teknolojia safi.

Mwelekeo wa Dira ya Taifa 2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 inalenga kujenga uchumi wa kisasa, wa viwanda, na wa kidijitali. Sekta ya madini ni moja ya nguzo za kufanikisha hilo kwa kuimarisha:

- Uongezaji thamani ya madini nchini
- Ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa uzalishaji
- Uzalishaji wenye tija, usalama, na endelevu

Kwa miradi kama Nyanzaga, Tanzania inaonesha uwezo na nia ya dhati ya kuwa **kitovu cha madini Afrika** na mchezaji muhimu katika uchumi wa dunia.

Faida kwa Jamii na Taifa

Mbali na mapato ya serikali kupitia kodi, mrabaha, na gawio, Nyanzaga pia umejipanga kuchangia maendeleo ya jamii kupitia ajira na masuala mengine ya muhimu yanayogusa jamii.

"Zaidi ya shilingi trilioni moja, zinataraajiwa kuwekezwa kwenye mradi huu hatua ambayo itafungua fursa mpya za kiuchumi na kijamii kwa watanzania. Mradi huu unatarajia kutoa ajira za moja kwa moja na zisio za moja kwa moja na hivyo kupunguza changamoto ya ukosefu wa ajira na suala la ushiriki wa watanzania katika utoaji wa huduma na bidhaa mbalimbali linatiliwa mkazo na Serikali," anasisitiza Waziri wa Madini Mhe. Anthony Mavunde azizungumza wakati wa kusainiwa mkataba wa nyongeza.

Hitimisho

Mradi wa Nyanzaga ni mwanzo wa zama mpya ya uwekezaji mkubwa kwenye madini ya dhahabu. Kupitia usimamizi bora, sera thabiti, taifa linaonesha kuwa linaweza kulinda maslahi yake huku likivutia wawekezaji wa Kweli kama anavyohibitisha Mkurugenzi wa Kampuni Mama ya Perseus Bi Lee- Anne de Buin ambaye alisema anashukuru mazungumzo yaliyofanywa baina ya kampuni hiyo na Serikali yaliyopelekea kusainiwa kwa mkataba wa nyongeza hivyo kuruhusu kuanza kwa shughuli za ujenzi.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu kwa kuendeleza mahusianomazuri ya kidiplomasia yaliyosaidia kurahisisha mkachato wa uwekezaji huu, anasema Bruin.

Madini ni uchumi na maendeleo na safari hiyo imeanza upya na Nyanzaga.

#Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

MRADI WA MKUJU KUIWEKA TANZANIA KWENYE RAMANI YA URANI DUNIANI

Na Agrey Singo.



Kusini mwa Tanzania, katikati ya misitu minene ya Mkoa wa Ruvuma, historia mpya ya taifa inandikwa. Katika kijiji cha Mto Mkuju, Wilaya ya Namtumbo palipozoeleka kama maskani ya wakulima na wavuvi wadogo, sasa kumeibuka mwanga mpya wa matumaini, mwanga wa madini muhimu duniani: madini Urani (Uranium).

Julai 30, 2025, itabaki kuwa siku ya kukumbukwa. Siku ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alizindua rasmi Kiwanda cha Majaribio cha Uchenjuaji Urani, tukio lililohudhuriwa na wananchi, viongozi wa Serikali na wawekezaji wa kimataifa waliokuja kushuhudia mwanzo wa zama mpya hapa nchini. "Ni siku ya kihistoria kwa nchi yetu. Tanzania inaanza rasmi safari ya kuwa mzalishaji mkubwa wa madini ya urani duniani kwa mara ya kwanza katika kiwango hiki. Urani ni madini mkakati tuliyobarikiwa kuwa nayo, na mchango wake utaimarisha nafasi yetu katika sekta ya madini kimataifa," alisema Rais Samia kwa sauti ya matumaini.

Safari ya Ndoto Kubwa

Kwa muda mrefu, Sekta ya Madini nchini Tanzania imekuwa ikiongozwa na dhahabu, almasi, vito vingine na hivi karibuni uzalishaji wa kinywe (graphite). Lakini sasa, ni zamu ya urani madini ambayo yanatoa nishati ya nyuklia safi na ya uhakika yanatarajiwa kubadili simulizi ya Tanzania. Kwa uzalishaji unaokadiriwa kufikia tani 300,000 kwa mwaka, Tanzania inajiweka moja kwa moja kwenye orodha ya nchi 10 bora duniani zinazozalisha urani kwa wingi.

Ni hatua itakayobadilisha sio tu taswira ya Sekta ya Madini, bali pia uchumi mzima wa Taifa. Kwa hisa za Serikali zinazofikia asilimia 20, mapato ya takribani dola milioni 40 kwa mwaka yanatarajiwa kuingia moja kwa moja katika hazina ya taifa, fedha zitakazogharamia miradi ya maendeleo, elimu, afya na miundombinu.

Manufaa ya Mradi wa Mkuju

Mradi huu mkubwa wa kimkakati umebeba manufaa ya aina nyingi yenye kugusa taifa, jamii na hata dunia.

Mosi, mapato kwa Serikali

Kwa umiliki wa asilimia 20 ya hisa, Serikali inatarajiwa kupata takribani dola milioni 40 kila mwaka kupitia gawio, kodi, tozo na mrabaha. Hii ni injini muhimu ya kufadhili huduma za kijamii, miradi ya miundombinu, elimu na afya, hivyo kupunguza mahitaji ya mikopo.

Pili, ajira kwa Watanzania

Mradi unatarajiwa kuajiri maelfu ya Watanzania moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kuanzia wahandisi wa madini, wataalamu wa mazingira, mafundi, hadi watoa huduma mbalimbali. Vijana wa Ruvuma na mikoa ya jirani wanatarajiwa kuwa miongoni mwa wanufaika wakuu.

Tatu, teknolojia na Utafiti

Urani si madini ya kawaida. Kuchakata kwake kunahitaji teknolojia ya hali ya juu na utaalamu maalum. Mradi huo wa Mkuju unafungua fursa za mafunzo na utafiti kwa wataalamu wa ndani, kushirikiana na wawekezaji wa kimataifa, na hivyo kukuza uwezo wa ndani wa kisayansi na kiteknolojia wa taifa.

Nne, huduma kwa Jamii (CSR)

Kupitia Mradi ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (Corporate Social Responsibility - CSR), Kampuni inayosimamia mradi inapaswa kuchangia moja kwa moja katika kuboresha maisha ya jamii. Wananchi wa Namtumbo na maeneo jirani watanufaika na ukarabati wa miundombinu kama shule, zahanati, maji safi, barabara na miradi mingine ya kijamii. Hatua hii itasaidia kupunguza changamoto zilizopo vijijini na kuunganisha jamii na maendeleo ya taifa.

Tano, Nishati Salama na Mustakabali wa Dunia

Katika zama za mabadiliko ya tabianchi, dunia inahitaji nishati safi na yenye uhakika. Urani ndiyo msingi wa nishati ya nyuklia inayotajwa kama "low-carbon energy" (hii ni nishati yenye kiwango cha chini cha kaboni) ni nishati inayozalishwa kwa njia zinazotoa gesi chache sana za ukaa (CO₂) au hazitoi kabisa, ikilinganishwa na mafuta ya kisukuku kama makaa ya mawe, gesi asilia, na mafuta ya petroli).

Hivyo, Tanzania, kupitia mradi wa Mkuju, inakuwa sehemu ya suluhisho la changamoto za nishati duniani, huku ikiheshimika kama mshirika wa maendeleo endelevu.

Mradi wa Mkuju si mradi wa kawaida. Ni kioo cha ndoto za Watanzania, daraja la teknolojia mpya, chanzo cha mapato na ishara ya uthubutu wa taifa.

Kama dhahabu ilivyoipa Geita jina kubwa duniani, sasa urani ya Mkuju inaiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia na safari mpya kama kinara wa nishati safi.

Vision 2030: Madini ni Maisha na Uajiri

MKATABA WA TGC, THAILAND WAANZA KUZAA MATUNDA

Na Asteria Muhozya



Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Thailand kupitia Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC) na Taasisi ya Jemolojia na Usonara (GIT) ya nchini Thailand yaliyosainiwa Februari 22, 2024 yameanza kuzaa matunda kufuatia uongozi wa juu wa GIT kuitembelea TGC na kufanya mazungumzo ya utekelezaji wa mkataba huo.

Kufuatia ziara hiyo, GIT iliishauri TGC kuhusu ununuzi wa vifaa vya maabara vinavyohitajika katika shughuli za uongezaji thamani madini ya vito ili kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango vya kimataifa. Pia, ilikubalika kufanya utafiti wa pamoja kwenye vito vya rangi pamoja na madini ya Tanzanite yaliyochomwa na ambayo hayajachomwa ili kuyatofautisha na kujua thamani halisi.

Mbali na kutembelea TGC, ujumbe wa Thailand ulikutana na wafanyabiashara wa madini ya vito jijini Arusha na wadau wengine wa Sekta ya Madini na kuwapatia ushauri wa namna ya kuyafikia masoko ya Kimataifa ya madini ya vito.

Maeneo mengine yaliyokubalika kupewa msukumo wa ushirikiano huo kuwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi na wanafunzi ikiwemo kubadilishana wataalamu, uboreshaji wa maabara ili kufikia viwango vinavyotambulika kimataifa, ushirikiano kwenye masuala ya utafiti na maendeleo kuhusu vito vya rangi vya Tanzania na ushirikiano kwenye kuandaa, kutangaza na kushiriki kwenye maonesho ya kimataifa ya madini ya vito.

Kuwasili kwa ujumbe wa GIT nchini ukiongozwa na Mtendaji Mkuu Bw. Sumed Prasongpongchai, ni hatua muhimu ya kuanza utekelezwa Makubaliano hayo (MoU), ambayo yanalenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika sekta Madini.

Lengo kuu la ziara hiyo lilikuwa kupata uelewa wa moja kwa moja kuhusu uwezo wa kiutendaji wa TGC pamoja na mazingira ya jumla ya biashara ya vito na usonara nchini.

Aidha, ziara ya GIT nchini inafuatia kikao cha awali kilichofanyika mwezi Februari, 2025, wakati wa Maonesho ya 71 ya Kimataifa ya Madini ya Vito na Usonara jijini Bangkok Thailand, ambapo katika kikao hicho, ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Katibu Mkuu Wizara ya Madini Eng. Yahya Samamba ulitembelea GIT na kufanya mazungumzo, ziara hiyo ililenga kusukuma mbele utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa mwaka 2024.

Mwaka 2024, Tanzania na Thailand zilisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika maeneo ya uhuilishaji teknolojia za kisasa, kuongeza ujuzi, tafiti, uimarishaji huduma za maabara za Madini ya Vito na metali, kubadilishana uzoefu kwa wakufunzi na wanafunzi pamoja na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa viwango vya kimataifa zinazotokana na madini ya vito ya thamani kubwa ambapo kwa upande wa Tanzania, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Madini Msafiri Mbibo alisaini kwa niaba ya Katibu Mkuu.

Jitihada hizo ni matokeo ya

utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Madini 2010 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2017, ambayo inataka madini kuongezwa thamani hapa nchini kabla ya kuuzwa nje ili kuzuia kupotea kwa fursa zinazotokana na shughuli za uongezaji thamani madini ikiwemo ajira, fedha za kigeni, n.k.

Tanzania inatajwa kuwa na zaidi ya aina 100 za madini ya vito, hivyo, ushirikiano huo unatarajia kuleta tija katika nyanja nyingi ikiwemo ya kuzalisha wataalamu wa ndani watakaokuwa na ujuzi wa kuzalisha bidhaa zitakazoweza kushindana kwenye masoko ya kimataifa.

Nchi ya Thailand tayari imepiga hatua kubwa kwenye shughuli za uongezaji thamani madini duniani ikiwemo kuzalisha ajira na kuingiza fedha za kigeni. Kwa Tanzania, ushirikiano huo ni eneo la uongezaji thamani madini ya vito kwani tayari imetenga shilingi bilioni 35 za ujenzi wa kituo cha pamoja kwa ajili ya shughuli za uongezaji thamani madini ya vito nchini, ambapo hadi sasa tayari shughuli za ujenzi zinaendelea jijini Arusha.

Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito na miamba pamoja na utengenezaji wa bidhaa za usonara katika kuanzia ngazi ya astashahada hadi stashahada (Diploma) katika fani mbalimbali huku tayari wahitimu hao wameshaanza kuajiriwa

Uongezaji thamani madini

ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 3 KUJENGA MAABARA ZA KISASA ZA MADINI NCHINI

Na Samwel Mtuwa

Katika juhudi za kuendeleza Sekta ya Madini nchini, Serikali kupitia Wizara ya madini imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya ujenzi wa maabara za kisasa zitakazojengwa katika mkoa wa Dodoma na mikoa ya kimadini ikiwemo mkoa wa Geita na Chunya kwa ajili ya kuhudumia shughuli za utafiti wa madini kama vile upimaji wa sampuli za miamba, madini na udongo kutoka kwa wadau mbalimbali wanaojishughulisha na shughuli za utafiti wa madini hususan kwenye uchimbaji na uchenjuaji.

Kutokana na umuhimu wa maabara hizo, tayari taasisi yenye dhamana hiyo ambayo ni Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) imeweka jiwe la msingi katika viwanja husika vitakavyojengwa maabara ikiwemo makao makuu ya maabara Dodoma pamoja na mkoani Geita ikiwa ishara ya kuanza rasmi ujenzi wa maabara hizo.

Ujenzi wa maabara hizo tatu utaipelekea Tanzania kuwa kitovu cha utafiti wa madini katika nchi za Afrika Mashariki na kati kwa kufanya tafiti zinazounganisha mfumo mzima wa jiosayansi ikiwemo utafiti wa Jiolojia na jiochemia kwenye upimaji wa sampuli za udongo, miamba, pamoja na utafiti wa mazingira kama vile sampuli za maji na mimea.

Kusogeza maabara hizi za kisasa katika maeneo ya karibu na shughuli za uchimbaji wa kimkakati kumetokana na tafiti nyingi zilizofanywa na GST kupitia wataalam wake katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za uchimbaji na kugundua kuwa kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa maabara za kisasa zenye teknolojia ya uchenjuaji wa madini hususan madini ya dhahabu ambayo upelekea upotevu mkubwa wa rasilimali hiyo inayoachwa kwenye marudio ya udongo pindi uchenjuaji unapofanyika jambo linalompelekea mchimbaji mdogo na wa kati kupoteza muda, mtaji pamoja na kuachia maeneo yenye uwepo wa rasilimali madini.

Kukamilika kwa maabara hizi katika maeneo husika itakuwa msaada mkubwa kwa wachimbaji na wachenjuaji madini, maana pamoja na kupata huduma kupitia maabara hizo pia wataalam watatoa elimu kuhusu namna bora ya uchenjuaji na uchukuaji wa sampuli kwa kuzingatia tabia ya mbale katika maeneo yanayochimbwa madini na kufanya uchimbaji kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Yote haya yanafanyika kwa kuzingatia dhima ya GST inayoelezea kuwa, moja ya jukumu lake kubwa katika Sekta ya Madini ni kutoa data na taarifa za jiosayansi zenye ubora wa hali ya juu na huduma kwa gharama nafuu kwa Serikali na wadau mbalimbali ili kuwezesha kufanya maamuzi ya kimkakati kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali madini; uratibu wa majanga ya asili ya Jiolojia ili kupunguza athari zake kwa kutoa elimu na ushauri; na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Kwa mujibu wa historia, maabara ya GST ilianzishwa mkoani Dodoma mwaka 1926 na Serikali ya kikoloni ya Uingereza iliyojulikana kama British Overseas Management Authority - (BOMA).

Kwa kipindi chote maabara hii imekuwa ikitoa huduma zake kutokea mkoani Dodoma tangu kuanzishwa kwake takribani miaka 100.

#Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri



STAMICO YAINGIA RASMI KWENYE UWEKEZAJI MKUBWA NCHINI

Na Tito Mselem



Katika kijiji kidogo cha Sesenga, kilichopo Wilaya ya Morogoro, historia mpya imeandikwa. Siku ya Julai 24, 2025 itasalia kuwa kumbukumbu ya kipekee kwa wakazi wa eneo hili, baada ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kukabidhiwa rasmi Leseni Kubwa ya Utafiti na Uchimbaji wa Madini ya Rare Earth Elements (REE) ambayo ni madini adimu yenye thamani kubwa katika soko la dunia na kulifanya shirika hilo kuingia kwenye uwekezaji mkubwa nchini.

Makabidhiano hayo yalifanyika katika hafla ya hadhara kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Sesenga, ambapo Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde, amekabidhi rasmi leseni hiyo kwa STAMICO, kufuatia maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika juhudi zake za kukuza uwekezaji wa kitaifa kwenye madini mkakati.

Kwa muda mrefu, vilima vya Wigu vilifahamika tu kama sehemu ya mandhari ya kijiji. Lakini sasa, vinageuka kuwa kitovu cha matumaini, ajira, na maendeleo. Madini ya Rare Earth Elements, ambayo yanapatikana eneo hilo, ni kati ya malighafi muhimu zaidi duniani leo, yakitumika katika utengenezaji wa vifaa vya teknolojia ya kisasa kama simu janja, kompyuta, magari ya umeme, mashine za tiba, hadi vifaa vya kijeshi.

"Haya si madini ya kawaida. Ni madini ya kimkakati yanayohitajika kwa kiwango kikubwa sana duniani. Sasa ni zamu ya Sesenga, Morogoro, na

Tanzania kwa ujumla kunufaika," anasema Waziri Mavunde huku akishangiliwa na wananchi waliokusanyika kwa wingi.

Kupitia leseni hii, STAMICO sasa inajitokeza rasmi kama mwekezaji mkubwa wa ndani katika uchimbaji wa madini adimu. Hili linaendana moja kwa moja na maono ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia, ya kuhakikisha rasilimali za taifa zinawanufaisha Watanzania na kuchochea maendeleo ya uchumi wa ndani.

Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dkt. Venance Mwasse, anaipongeza Serikali kwa kuendelea kuwaamini na kuwapa nafasi ya kipekee kushiriki moja kwa moja katika miradi mikubwa ya madini.

"Tunaichukulia hii kama dhamana kubwa kwa Taifa. Tupo tayari kuanza kazi mara moja, kwa weledi wa hali ya juu, kuhakikisha mradi huu unaleta matokeo chanya kwa wananchi wa Morogoro na taifa kwa ujumla," anasema Dkt. Mwasse.

Mradi huu unatarajiwa kuwa chachu ya mageuzi ya kiuchumi katika Wilaya ya Morogoro. Waziri Mavunde anaeleza kuwa STAMICO inatakiwa kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa wananchi wa eneo hilo kwa ajira, uuzaji wa bidhaa, huduma na ushirikishwaji kupitia mpango wa "Local Content".

Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro itanufaika moja kwa moja kupitia makusanyo ya kodi na tozo mbalimbali kutoka kwenye shughuli za uchimbaji madini.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mhe. Mussa Kilakala, anaeleza faraja yake akisema: "Ni heshima kwa Morogoro kuwa sehemu ya historia hii. Tutaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu ili matokeo yake yasiishie kwenye makaratasi tu, bali yadhihirike katika maisha ya watu wetu."

Leseni hiyo inakabidhiwa STAMICO baada ya Serikali kufanikisha kuirejesha kutoka kwa kampuni ya Wigu Hill Mining Company Limited, kufuatia kumalizika kwa shauri katika Baraza la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji. Hili linaashiria dhamira thabiti ya Serikali ya kuhakikisha maeneo yenye rasilimali hayakai bila kuendelezwa, na kwamba miradi yote ya madini inaleta manufaa halisi kwa taifa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Mhandisi Yahya Samamba, anasisitiza umuhimu wa mazingira salama na rafiki kwa uchimbaji nchini, huku akimpongeza Rais Dkt. Samia kwa kuendelea kuweka msingi thabiti wa mageuzi katika sekta ya madini.

Leseni hii kwa STAMICO ni zaidi ya hati ya kisheria ni mlango wa matumaini. Ni ushahidi kuwa Tanzania sasa inapiga hatua za makusudi kuelekea umiliki wa rasilimali zake kwa faida ya watu wake. Ni mwanzo wa hadithi mpya ya mafanikio kwa wananchi wa Sesenga, na ni mfano halisi wa Sera za Dkt. Samia kuanza kuzaa matunda.

Kwa sasa, STAMICO imepewa dhamana na Watanzania wanasubiri kuona matokeo.

CHUMVI: MADINI MUHIMU KIAFYA NA FURSA YA KIMKAKATI KWA UCHUMI WA TAIFA

Na Tito Mselem



Chumvi ni madini ya asili yenye umuhimu mkubwa kwa maisha ya kila binadamu na pia ni rasilimali yenye fursa kubwa ya kiuchumi nchini Tanzania. Kwa upande wa kiafya, chumvi huchangia katika kazi mbalimbali za mwili kama vile kudhibiti uwiano wa maji mwilini, kusaidia misuli kufanya kazi, pamoja na kurahisisha mawasiliano ya neva kupitia upitishaji wa ishara za umeme.

Mbali na umuhimu huo wa kiafya, chumvi pia ni zao lenye mchango mkubwa kiuchumi, hasa kwa wakazi wa maeneo yenye uzalishaji kama vile Uvinza, Pangani na maeneo ya pwani.

Tanzania ina maeneo mengi yanayoweza kuzalisha chumvi kwa wingi kupitia njia za asili kama uvukizaji wa maji ya bahari au maji ya chumvi ardhini. Hii ni fursa kubwa ya biashara na ajira, hasa kwa vijana na wajasiriamali, kwani chumvi hutumika si tu kwa matumizi ya nyumbani bali pia viwandani katika utengenezaji wa sabuni, ngozi, na usindikaji wa vyakula. Ikiwekezwa vizuri, sekta hii inaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa na kusaidia katika kupunguza uagizaji wa chumvi kutoka nje ya nchi.

Kutokana umuhimu huo, timu ya Madini Diary kutoka Wizara ya Madini inafunga safari mpaka katika

Kiwanda cha Tansalt kilichopo mkoani Tanga ambacho kimekuwa msaada mkubwa kwa wachimbaji na wakulima wa chumvi nchini kwa kusaidia kuwapatia uhakika wa soko la bidhaa hiyo, hatua ambayo imechangia kukuza kipato cha wazalishaji wadogo na kuongeza thamani ya chumvi katika masoko ya ndani.

Katika jitihada za kukuza uchumi wa viwanda na kuinua kipato cha wachimbaji wadogo wa madini nchini, Kiwanda hicho kimejidihirisha kuwa nguzo imara ya mageuzi katika sekta ya uzalishaji na usindikaji wa chumvi. Kupitia uwezo wake mkubwa wa kuchakata chumvi ghafi na kuibadilisha kuwa bidhaa yenye thamani kubwa sokoni, Tansalt si tu kwamba kimekuwa kiwanda kinachotegemewa na wakulima wa chumvi, bali pia ni chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika ukanda wa pwani na Tanzania kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Tanga, Mhandisi Laurent Bujashi, anasema kwa miaka mingi wachimbaji wa chumvi wamekuwa wakikumbwa na changamoto ya kutopata soko la uhakika kwa bidhaa zao, jambo lililosababisha bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei duni isiyokisi nguvu kazi na gharama za uzalishaji.

Hali hiyo imebadilika kufuatia uwepo wa Tansalt, kiwanda ambacho kimeimarisha mnyororo wa thamani

wa chumvi kwa kununua malighafi kutoka kwa wazalishaji wadogo na kuisindika hadi kufikia viwango vinavyokubalika katika masoko ya kitaifa na kimataifa.

“Kupitia Tansalt, wachimbaji wa chumvi sasa wanapata soko la uhakika kwa bidhaa zao, hali inayosaidia kuongeza kipato chao, kuhamasisha uzalishaji endelevu, na kuchochea ukuaji wa uchumi wa mkoa wa Tanga,” alisema Mhandisi Bujashi.

Faida za kiwanda hicho hazijaishia tu kwenye ununuzi wa chumvi ghafi. Uwepo wa Tansalt umechangia pia katika utoaji wa ajira kwa wakazi wa eneo hilo, kuibua fursa mpya za biashara ndogo ndogo, kuimarisha shughuli za usafirishaji wa bidhaa, na kusaidia utoaji wa huduma za kijamii. Aidha, chumvi yenye iodini inayozalishwa kiwandani hapo imekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na maradhi yanayotokana na upungufu wa madini ya iodini, tatizo ambalo limekuwa likiathiri hasa watoto na wanawake nchini.

Vision2030: Madini ni Maisha na Utajiri.

MADINI YANAPOGEUKA MBOLEA: SAFARI YA KUUNGANISHA MIGODI NA MASHAMBA

Na Agrey Singo.



Jinsi Madini Yanavyobeba Siri ya Rutuba Shambani.

Tanzania inapoendelea kuijenga ajenda yake ya uchumi wa viwanda, simulizi moja kutoka Tanga inatoa funzo la kipekee kuhusu namna Sekta ya Madini inapofungamanishwa na Sekta nyingine kama kilimo kwa manufaa ya taifa. Simulizi hii inazungumzia zaidi ya mawe na udongo bali ni simulizi ya maisha, upatikanaji wa chakula, ajira na malengo ya taifa.

Jinsi Madini Yanavyobeba Siri ya Rutuba Shambani.

Kwa kawaida, Sekta ya Madini imekuwa ikiangaliwa kama injini ya mapato ya kigeni kupitia dhahabu, almasi, tanzanite, vito vingine, makaa ya mawe na nengineyo. Lakini kwa undani zaidi, madini ya viwandani kama dolomite, chokaa (limestone), gypsum (jasi) na phosphate yanaibuka kama "madini ya kimya" yanayochochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo.

Kwa mujibu wa Rishit Lalseta, Mkurugenzi wa Kiwanda cha Tanga Mining Limited:

"Dolomite ni nyenzo muhimu kwenye utengenezaji wa mbolea. Inaongeza kalsiamu na magnesiamu kwenye udongo, inapunguza tindikali, na kufanya mazao kukua kwa afya na kutoa mavuno bora."

Kwa lugha rahisi, kilichokuwa jiwe lenye thamani chini ya ardhi, kinapogeuka kuwa mbolea, kinakuwa dawa ya udongo na chanzo cha uzima wa mazao, mavuno mengi zaidi, na uhakika wa chakula.

Daraja Kati ya Sekta Mbili

Sekta ya Madini na Sekta ya Kilimo, kwa muda mrefu zilionekana kana kwamba zinatembeka barabara tofauti. Moja ikihusishwa na ardhi kuchimbwa, nyingine ikihusishwa na ardhi kulimwa. Lakini leo, daraja la moja kwa moja limejengwa Sekta ya Kilimo ikitegemea kulishwa na Madini huku Sekta ya Madini ikiongeza tija kupitia malighafi hiyo.

Madini yanatoa malighafi (kama dolomite na phosphate), viwanda vya mbolea vinabadilisha malighafi kuwa bidhaa, wakulima wanazalisha mazao bora zaidi kutokana na bidhaa hizo. Huo ni mnyororo wa thamani unaounganisha mgodi na shamba, mchimbaji na mkulima, ajira za viwandani na usalama wa chakula.

Kwa maneno ya Lalseta:

"Soko la mbolea nchini bado ni kubwa, na mahitaji ni makubwa sana. Hivi sasa tunahudumia ndani ya nchi, lakini tunapanga kusogea kimataifa, ili bidhaa zetu zisaisaidie tu kilimo cha Tanzania, bali pia kuingiza fedha za kigeni."

Kiwanda cha Tanga Mining kilipoanza mwaka 2014, kilikuwa kama cheche ndogo. Leo hii, matokeo yake yanaonekana wazi:

- Ajira: Mamia ya wananchi wa Tanga na mikoa jirani wamepata kazi,
- Mapato ya serikali: Kodi na tozo zimeongezeka,
- Kilimo chenye tija: Wakulima wanaopata mbolea zenye virutubisho vya dolomite wanavuna zaidi na bora,
- Usalama wa chakula: Taifa linapata uhakika wa chakula kutokana na ongezeko la tija.

Mhandisi Laurent Bujashi, Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Tanga, anasema:

"Tunaposhuhudia dolomite ikitumika kutengeneza mbolea, maana yake tunaleta suluhisho la changamoto za kilimo na usalama wa chakula. Hii ni njia ya kuhakikisha wananchi wananufaika moja kwa moja kupitia sekta za kilimo, viwanda na ujenzi."

Kauli hii inaonesha dhamira ya Serikali: kuchukua madini kutoka ardhi, kuyabadili kuwa bidhaa, na hatimaye kuyageuza kuwa nguzo ya maisha bora kwa wananchi.

Maono ya Mbeleni

Sekta ya Madini ikichangia kwenye kilimo, faida si kwa mkulima pekee, taifa linapata chakula cha kutosha, wakulima wanapata mavuno yenye faida zaidi, Serikali inapata mapato ya kodi, uchumi wa viwanda unapata nguvu mpya.

#Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri

GESI YA HELIUM KUWA MKOMBOZI UCHUMI WA VIWANDA TANZANIA

Na Samwel Mtuwa

Sekta ya Viwanda ndio chimbuko la maendeleo ya haraka ya nchi mbalimbali na ni mhimili mkuu wa kutegemewa katika kuongeza thamani ya malighafi tulizonazo, kutoa ajira kwa wananchi na kuongeza mapato ya Serikali, fedha za kigeni pamoja na kuongeza na kuboresha sayansi na teknolojia.

Katika kuakikisha hayo yanafanikiwa Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu imekuwa ikifanya tafiti zake mbalimbali kwa lengo la kugundua rasilimali mpya zitakazo chochea maendeleo ya kiuchumi wa viwanda nchini.

Baada ya utafiti wa mda mrefu wataalamu wa utafiti wa madini nchini wamefanikiwa kugundua gesi ya helium ambayo ni moja ya gesi adimu duniani, ambapo kwa mujibu wa tafiti mbalimbali zilizofanyika imegundulika kuwa Tanzania ina aina mbalimbali za gesi asilia, kama vile helium, zikionesha uwepo wa hifadhi ya futi za ujazo bilioni 138 kwenye Bonde la Ziwa Rukwa, ambazo zinaweza kutumika kwa kipindi cha zaidi ya miaka ya 20.

Sambamba na tafiti mbalimbali zilizokwisha fanyika, kampuni ya

HeliumOne nchini Tanzania imefanikiwa kugundua gesi hiyo katika umbali wa kilomita 1.14 kutoka chini ya ardhi katika visima vya Itumbula West 1 na Tai 3 ikionesha kuwa na wingi wa mkusanyiko wa gesi ya helium hiyo yenye ubora wa kiwango cha asilimia 7.9 jambo lililoleta matumaini ya kuendelea na utafiti wa kina.

Kijiolojia gesi ya helium inaweza kupatikana katika kina kifupi au kirefu hii inatokana na Jiolojia ya sehemu husika ikiwa na matumizi mbalimbali kama vile hutumika katika vifaa vya umeme mfano radio, teknolojia ya mawasiliano ya baluni angani, urushaji wa helikopta (Chopa), kupunguza uzito wa mafuta ya ndege, kutengeneza taa mfano taa aina ya tubelight pamoja na kuendesha mashine za kupiga picha hospitalini za MRI Scanner.

Kabla ya ugunduzi huo watafiti walikuwa wamebashiri ukosefu wa gesi hiyo baridi ifikapo mwaka wa 2035, hivyo kupelekea wataalamu kuhimiza kutungwa kwa sheria itakayopunguza matumizi yake katika bidhaa zisizo za dharura kama vile kwenye mashine maalum kutokana na hali ya kuwa gesi hiyo ya Helium ni nyepesi kuliko ile ya Oxygen.

Hivyo kugundulika kwa helium mkoani Rukwa inatajwa kama hazina kubwa zaidi duniani ikitegemewa kuziba pengo la upungufu wa helium lililokuwa likitishia kupotea kwa gesi hiyo kwa sababu matumizi na mahitaji yake yanaongezeka katika teknolojia mbalimbali za kimkakati.

Kwa mujibu wa Tovuti ya taasisi inayoshughulika na masuala ya Jiosayansi nchini Marekani (USGS) inaonyesha kuwa soko la helium duniani linatarajiwa kuongezeka kufikia kiasi cha dola za Marekani bilioni sita kwa mwaka.

Kulingana na takwimu za uzalishaji, Marekani ndiye msambazaji mkubwa wa gesi ya helium duniani ikiwa na asilimia 60 za uzalishaji, ikifuatiwa na Qatar ina asilimia 24, na wasambazaji wengine ni pamoja Algeria, Australia, Canada na Urusi.

Taarifa ya kampuni inayosimamia matumizi ya gesi asilia ijulikanayo kama great plain ya nchini Australia imeonesha kuwa ugunduzi wa gesi kwa kiasi hicho kinaweza kujaza mitungi ya kifaa cha kupimia matibabu yaani (MRI) zaidi ya milioni 1.2.



KUTOKA ARDHINI HADI HAZINA: SAFARI YA TANZANIA KUWA KINARA WA DHAHABU AFRIKA

Na Asteria Muhozya

Kwa miaka mingi, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zenye shughuli nyingi za uchimbaji wa dhahabu barani Afrika tangu kabla ya uhuru hadi sasa. Hivi sasa dhahabu inachangia kiasi kikubwa katika uchumi na maendeleo ya taifa ambapo asilimia 80 ya mapato ya madini nchini yanatokana na dhahabu.

Hata hivyo, kwa kipindi kirefu Tanzania haikuwa na hifadhi rasmi ya dhahabu licha ya madini hayo kuwa chanzo kikuu cha mapato ya Sekta ya Madini. Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Kifungu cha 59 yaliyofanywa mwezi Julai, 2024, yalitaka kila leseni ya kusafirisha dhahabu nje ya nchi kutenga asilimia 20 ya uzalishaji wake kwa ajili ya kuuza ndani ya nchi kupitia Benki KUU ya Tanzania iliyopewa haki ya kwanza ya ununuzi.

Mwezi June mwaka 2025, Serikali kupitia BoT ikasaini mkataba na kampuni kubwa za uchimbaji dhahabu za Geita Gold Mining Limited (GGML), Buckreef Gold yenye ubia na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) pamoja na kiwanda cha Kusafisha dhahabu cha Geita Gold Refinery (GGR) ili kurahisisha ununuzi na usafirishaji wa dhahabu.



Uamuzi huo wa Serikali unalenga kuongeza akiba ya taifa ya fedha za kigeni ikiwa ni sehemu ya kuimarisha uchumi wa nchi na kuhakikisha thamani ya madini inabaki nchini. Kwa msingi huo wa kisera, Tanzania inashika nafasi kubwa kufikia kilele cha hifadhi za dhahabu barani Afrika.

Aidha, hatu hiyo ya BoT inawaweka wachimbaji urahisi wa kufanya biashara kwa kuwa sasa wanaweza kuuza hadi asilimia 100 ya dhahabu kwenye benki hiyo. Uuzaji huo wa dhahabu unafanyika kupitia viwanda vitatu vya kusafisha dhahabu vyenye mkataba na Serikali vya Geita Gold refinery (GGR) kilichopo mkoani Geita, Africa Eyes Refinery kilichopo Geita, Mwanza Precious Metals Refinery chenye ubia na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kilichopo jijini Mwanza na Eyes of Afrika ya Dodoma. Tayari Tanzania inavyo viwanda vinane na Kusafisha dhahabu.

Kufuatia uamuzi huo wa Serikali, ndani ya kipindi cha muda mfupi sana kuanzia Oktoba 2024 hadi sasa tayari Tanzania imekusanya tani 10 za dhahabu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.5, ikiwa ni mkakati wa kuimarisha akiba ya taifa na kulinda uchumi dhidi ya misukosuko ya kimataifa. Kiasi hicho cha akiba ya dhahabu kinafanya Tanzania kuwa mbele

ya Msumbiji yenye tani 3.869 ambayo awali ilihesabika kama nchi ya 10 kwa ubora Afrika wa uhifadhi wa dhahabu Afrika, zikitanguliwa na Algeria yenye tani 174.

Mafanikio haya ni matokeo ya maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyehamiria kulinda rasilimali na kuimarisha uchumi hususan nyakati za changamoto kama uhaba wa dola na misukosuko ya kifedha lakini pia ni dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha rasilimali madini inawanufaisha watazania na taifa lote.

Kwa hatua hizi thabiti na maamuzi ya kimkakati, Tanzania inaendelea kuandika historia mpya katika sekta ya madini, si tu kama mzalishaji mkubwa wa dhahabu, bali pia kama nchi inayotunza na kuhifadhi thamani ya rasilimali zake kwa faida ya wananchi wake.

Kwa uongozi makini wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, taifa limejipambanua kama mfano wa kuigwa barani Afrika katika kulinda maslahi ya kiuchumi kupitia dhahabu. Ni dhahiri kuwa Tanzania ya leo inajenga msingi imara wa kesho iliyo bora, yenye uchumi thabiti, na heshima katika jamii ya mataifa duniani kupitia Sekta ya Madini

Vision 2030: Madini ni Maisha na Utajiri



TANZANIA KUNUFAIKA NA MADINI YA URANIUM

Na Samwel Mtuwa

Kwa muda mrefu sasa Tanzania imekuwa ikitambuliwa kama moja ya nchi yenye rasilimali nyingi za madini yakiwemo madini ya metali, vito, ujenzi, viwanda, madini ya nishati, madini adimu (REE) na madini ya kimkakati, ndoto ya miaka mingi inakwenda kutimia mbele ya macho yetu baada ya aina mpya ya madini ya nishati kugundulika nchini na kuanza majaribio ya uchenjuaji ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi nayo ni madini ya Urani.

Eneo la Mkuju, Namtumbo ni mojawapo ya maeneo machache yenye akiba kubwa ya madini ya uranium, jambo linaloifanya Tanzania kuwa kitovu cha kuvutia wawekezaji wa kimataifa katika Sekta ya Madini hususan madini haya ya kimkakati. Akiba ya uranium katika eneo hili inakadiriwa kufikia tani milioni 139, hii inaweza kuiweka Tanzania miongoni mwa nchi 10 bora duniani zenye uwezo mkubwa wa uzalishaji.

Mradi mpya wa uranium katika eneo la Mkuju River, wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma ni mradi unaotarajiwa kuwa na uwezo wa uzalishaji wa miaka 22, na kuchangia hadi 4% ya uzalishaji wa uranium duniani.

Serikali ya Tanzania imedhihirisha dhamira yake ya kuimarisha sekta ya madini kwa kuweka mazingira bora ya uwekezaji kupitia sera na mifumo ya kodi inayowavutia wawekezaji. Miundombinu kama bandari za Dar es Salaam na Mtwara ni nguzo muhimu katika usafirishaji wa madini haya kwenda masoko ya kimataifa.

Zaidi ya faida ya kimataifa, mradi huu ni chanzo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma unatarajiwa kuongeza mapato ya serikali, kuleta ajira kwa maelfu ya Watanzania, na kuchochea shughuli za biashara na huduma katika maeneo jirani.

Tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa rai kwa kampuni ya Mantra Tanzania Limited kuzingatia ushirikishwaji wa watanzania katika utoaji wa huduma mbalimbali migodini kwa mujibu wa sheria ya madini ya mwaka 2010, na kuitaka Wizara ya Madini na taasisi zote zinazohusika kuhakikisha mradi unakuwa shirikishi, endelevu na wenye manufaa makubwa kwa Taifa.

Anatoa rai hiyo wakati akizindua kiwanda cha majaribio cha kuchenjua urani wilayani Namtumbo na mradi huo ukitajwa kuwa mkubwa na wa kipekee ukanda wa Afrika Mashariki

